TANGAZO LA SERIKALI Na. 506 la tarehe 21/05/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI),
(SURA YA 288)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 89(1))*

SHERIA NDOGO YA UDHIBITI NA USIMAMIZI WA MIFUGO YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"afya" maana yake ni hali timilifu ya kimwili na kiakili ya mnyama;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni;

"kero au chukizo" maana yake ni kitu chochote ambacho kipo katika hali yoyote iwe kinatumika, kimewekwa, kimejengwa au ni kichafu kiasi cha kusababisha-

(a) hatari kwa viumbe na maisha ya binadamu;
(b) harufu mbaya ya kuudhi;

(c) kuzaliana kwa wadudu na wanyama hatari kama vile inzi, mende, sisimizi, panya, nyoka, nyuki, kunguni au viumbe wengine hatari; au
(d) magonjwa kwa binadamu, kuhifadhi mbu, inzi, panya na viumbe wenye madhara;

"kibali" maana yake ni idhini ya maandishi inayotolewa na Halmashauri kwa ajili ya kufanya shughuli iliyokusudiwa chini ya Sheria Ndogo hii;

"mfugo" maana yake ni ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku au mnyama mwingine anayefugwa;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya kinondoni au afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

Wajibu wa Halmashauri

4. Halmashauri itakuwa na wajibu wa-
(a) kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi;
(b) kuelekeza idadi ya mifugo ambayo kila mfugaji anaruhusiwa kufuga kulingana na ukubwa wa eneo lake;
(c) kwa kushirikiana na wananchi, kujenga majosho ya mifugo;
(d) kutoa elimu ya ufugaji bora kwa jamii ili kuongeza tija;
(e) kufanya sensa ya mifugo, kuweka alama na kutoa kadi za mifugo;
(f) kwa kushirikiana na wafugaji, kutoa chanjo ili kudhibiti magonjwa ya mifugo yasiyoambukiza na yanayoambukiza binadamu; na
(g) kudhibiti uzururaji holela wa mifugo na wanyama katika Halmashauri kwa mujibu wa Sheria.

Wajibu wa mfugaji

5. Kila mfugaji chini ya Sheria Ndogo hii atakuwa na wajibu wa-

(a) kuogesha mifugo yake ili kudhibiti magonjwa ya wanyama kama atakavyoelekezwa na Halmashauri;

(b) kupeleka mifugo yake katika vituo vya chanjo kama itakavyoamriwa na Halmashauri na atalipia chanjo hiyo ikiwa atatakiwa kufanya hivyo kwa kuzingatia viwango vitakavyoainishwa na mamlaka husika;

Sura ya 184

(c) kuhakikisha mifugo yake inawekwa alama maalumu zinazotolewa kwa mujibu wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo;

(d) kufuga idadi ya mifugo katika jengo lililoidhinishwa kulingana na maelekezo yaliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza;

(e) kuwa na kadi ya mifugo inayoonesha idadi na aina ya mifugo aliyonayo;

(f) kuipa mifugo yake malisho au chakula na maji ya kutosha kwa kuzingatia kanuni bora za ufugaji;

(g) kuwa na kibali cha kusafirisha mifugo na mazao yake;

(h) kufuga kwa kuzingatia mipango ya matumizi bora ya ardhi;

(i) kuhudhuria mafunzo ya ufugaji kadri itakavyohitajika na Halmashauri; na

(j) kuuza mifugo yake katika masoko na minada iliyoidhinishwa au eneo lingine kwa taarifa maalumu.

Kibali cha kufuga wanyama

6.-(1) Mtu anayekusudia kufuga mifugo atalazimika kupata kibali cha kufuga kutoka Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(2) Ada ya kibali cha kufuga itakuwa shilingi elfu kumi.

(3) Bila kujali kanuni ndogo ya (2), endapo mtu atakiuka taratibu za ufugaji zilizoainishwa katika Sheria

Ndogo hii, Halmashauri inaweza kufuta kibali chake na kumtaka kuhamisha mifugo yake yote.

Masharti kwa mfugaji

7. Mfugaji hataruhusiwa-
(a) kuchunga, kulisha au kunywesha maji mifugo katika maeneo ambayo hayakutengwa kwa shughuli hiyo;
(b) kusafirisha mifugo kwa kuiswaga barabarani;
(c) kusafirisha au kuhamisha mifugo kutoka eneo moja hadi lingine bila kibali kutoka Halmashauri;
(d) kuingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali;
(e) kuuza au kununua mifugo katika maeneo ambayo siyo ya mnada, masoko au magulio ya mifugo yaliyoaidhinishwa, bila kibali maalumu cha Halmashauri;
(f) kufuga mifugo zaidi ya idadi iliyoainishwa katika Sheria Ndogo hii; na
(g) kununua, kuuza au kufanya biashara ya kubadilishana aina yoyote ya mfugo katika eneo la Halmashauri bila kibali maalumu isipokuwa kwenye minada au magulio yaliyotengwa kwa shughuli hiyo na Halmashauri.

Kibali cha kusafirisha mifugo

8.-(1) Mtu anayekusudia kusafirisha mfugo au mazao yatokanayo na mfugo kutoka au kuingia katika eneo la Halmashauri atapaswa kuwa na kibali.

(2) Halmashauri itatoa kibali cha kusafirisha mifugo baada ya mfugaji kutoa uthibitisho wa kumiliki mfugo kutoka kwa Afisa Mwidhiniwa.

(3) Kibali cha kusafirisha mifugo au mazao yatokanayo na mifugo kitakuwa kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu.

(4) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa-

(a) kukagua kibali cha kusafirisha mfugo au mazao ya mifugo ili kujiridhisha kuhusu uzingatiaji wa Sheria Ndogo hii;

(b) kukamata mfugo au mazao ya mifugo yanayosafirishwa kinyume na Sheria Ndogo hii; na

(c) kutoza faini kwa mmiliki wa mfugo au mazao ya mifugo yanayosafirishwa kinyume na Sheria Ndogo hii kwa kuzingatia utaratibu ulioainishwa.

Kudhibiti mifugo inayozurura ovyo

10.-(1) Halmashauri itakamata mfugo utaoonekana unazurura ovyo katika eneo la Halmashauri.

(2) Mfugaji ambaye mfugo wake utakamatwa chini ya kanuni ndogo ya (1) atawajibika kulipa faini ya shilingi elfu kumi kwa kila siku.

(3) Endapo mfugo uliokamatwa hautachukuliwa na mmiliki ndani ya kipindi cha siku saba tangu kukamatwa, Halmashauri itakuwa na haki ya kuuza kwa mnada mfugo huo baada ya kupata idhini ya Mahakama, na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmliki wa mfugo huo baada ya kutoa faini inayodaiwa, gharama za kuhifadhi mfugo, gharama ya Mahakama na gharama ya mnada.

(4) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (3), kabla ya kuuza kwa mnada mfugo uliokamatwa, Halmashauri itatoa taarifa ya siku saba kwa mmiliki na umma kuhusu kusudio la kuuza mfugo huo.

(5) Endapo kwa sababu yoyote mfugo utakufa, Halmashauri haitawajibika na ulipaji wa gharama zozote isipokuwa kama kifo hicho kimesababishwa kwa uzembe wa watumishi wa Halmashauri.

Ukaguzi wa mifugo na mazao ya mifugo

11.-(1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kukataa aina yoyote ya mifugo au mazao ya mifugo kuingia au kuuzwa ndani ya eneo la Halmashauri, iwapo mifugo au

mazao ya mifugo husika yanaweza kuhatarisha afya au usalama wa mifugo mingine au watumiaji.

(2) Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika nyumba au jengo lolote kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni kwa lengo la kukagua utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

Taratibu za biashara ya mifugo na mazao yake

12.-(1) Mtu anayekusudia kuanza biashara ya mifugo na mazao ya mifugo atatakiwa kuwa na leseni, utambulisho na vibali kutoka Mamlaka husika vinavyohusu kuuza na kununua mifugo na mazao ya mifugo na kuwasilisha vibali hivyo Halmashauri kwa ajili ya uhakiki.

(2) Mfanyabiashara wa mifugo inayopelekwa au kutoka mnadani au machinjioni atatakiwa kuwa na kibali maalumu kutoka Halmasahauri.

(3) Mfanyabiashara atakayesafirisha mifugo kutoka nje ya Halmashauri atatakiwa kuwa na kibali kutoka Halmashauiri ambayo mifugo hiyo inatoka.

(4) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (2) na (3), mfanyabiashara wa mifugo atatakiwa kusafirisha mifugo katika vyombo vya usafiri vinavyokubalika kwa mujibu wa Sheria.

(5) Mifugo yote itauzwa au kununuliwa katika minada au masoko yanayotambulika kwa mujibu wa Sheria.

(6) Mtu atakayesafirisha mifugo bila kibali au kuuza katika eneo ambalo halijaidhinishwa kwa ajili ya shughuli hiyo, atalazimika kulipa faini ya shilingi elfu kumi kwa kila mfugo.

(7) Minada yote ya mifugo au magulio ya mifugo itafanyika kwa kibali maalumu cha Halmashauri na kwenye maeneo yaliyoruhusiwa.

Wajibu wa mfanyabiashara wa bucha na

13. Mfanyabiashara wa bucha au duka la nyama atakuwa na wajibu wa -

(a) kuwa na leseni na vibali vya kufanya biashara hiyo;

maduka ya nyama

(b) kuhakikisha kuwa jengo lake la biashara lina mwanga wa kutosha, umeme, maji safi na salama, visu, meza, mzani wa kawaida au mzani wa kielektroniki na misumeno maalumu ya kukatia nyama;
(c) kuwa na kabati la vioo la kuzuia inzi na wadudu wengine wataambao;
(d) kuwa na jokofu la kuhifadhia nyama;
(e) kuwa na pipa la kuhifadhia taka ngumu na laini;
(f) kuhakikisha kuwa nyama imekaguliwa na mkaguzi aliyeidhinishwa na kugongwa muhuri na inauzwa ndani ya jengo;
(g) kuhakikisha kuwa muuzaji anavaa sare nyeupe muda wote ambazo ni mabuti, koti na kofia;
(h) kuhakikisha kuwa muuzaji anapima afya yake kila baada ya miezi sita na kuhakikisha anakuwa na cheti cha upimaji; na
(i) kutoa ushirikiano kwa wakaguzi mara atakapotakiwa kufanya hivyo wakati wowote wa ukaguzi.

Usafirishaji wa nyama

14.-(1) Mfanyabiashara wa nyama atatakiwa kusafirisha nyama kutoka machinjioni kwa kutumia gari maalumu na endapo atatumia usafiri wa pikipiki au baiskeli atatakiwa kubeba nyama kwa kutumia chombo maalumu kilichoidhinishwa na Halmashauri.

(2) Mmiliki wa gari la kubeba nyama, pamoja na kulipia gharama za usafirishaji kama zilivyoainishwa na Halmashauri atahakikisha kuwa gari lake-

(a) limesajiliwa na kupewa cheti maalumu cha ukaguzi na Halmashauri;
(b) linakaguliwa kila baada ya miezi mitatu;
(c) lina sanduku la aluminiamu lenye mfuniko na limepakwa rangi nyeupe, mstari mwekundu na namba; na

(d) halibebi kitu kingine kinachoweza kuleta madhara au athari kwa afya ya mlaji.

Udhibiti wa uchinjaji machinjioni

15.-(1) Mtu anayehusika na shughuli za machinjio anapaswa kupima afya kila baada ya miezi sita.

(2) Mtu anayehusika na machinjio anapaswa kuwa wasafi, na kuvaa mavazi maalumu kwa ajili ya kazi hiyo.

(3) Hairuhusiwi kukaa au kufanya mkusanyiko wa aina yoyote katika eneo la machinjio isipokuwa kwa kibali maalumu kitakachotolewa na Halmashauri.

(4) Uendeshaji wa machinjio utazingatia sheria na taratibu za afya.

(5) Hairuhusiwi kufanya biashara ya aina yoyote katika eneo la machinjio.

(6) Hairuhusiwi kuweka bucha au duka la nyama au biashara yoyote ya nyama ndani ya mita mia mbili kutoka eneo la machinjio.

(7) Mfugaji atatakiwa kupeleka mfugo au mifugo yake machinjioni au mahali huduma hiyo inapopatikana na itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuchinja mfugo mahali pengine popote ambapo sio machinjio isipokuwa kwa kutoa taarifa kwa Afisa Mwidhiniwa na atalazimika kulipia gharama za machinjio kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

(8) Nyama haitaruhusiwa kutumika kwa matumizi ya binadamu bila kufanyiwa ukaguzi wa mwisho na kuwa na muhuri maalumu wa ukaguzi wa nyama.

(9) Mtu hataruhusiwa kuingiza mifugo katika machinjio kwa ajili ya kuchinja baada ya saa kumi na moja jioni isipokuwa kwa kibali maalumu cha Halmashauri.

(10) Mifugo haitaruhusiwa kuchinjwa bila kufanyiwa ukaguzi wa awali.

(11) Mtu anayehusika na shughuli za machinjio au anayeingia katika machinjio haruhusiwi kutumia lugha za kashfa, kuudhi, kudhalilisha au matusi katika eneo la machinjio.

Udhibiti wa ufugaji wa mbwa

16.-(1) Mtu hataruhusiwa kufuga mbwa katika eneo la Halmashauri bila kibali cha ufugaji kutoka Halmashauri.

(2) Kibali cha ufugaji mbwa kitalipiwa kiasi cha shilingi elfu kumi na kitadumu kwa kipindi cha mwaka mmoja.

(3) Mfugaji wa mbwa atakuwa na wajibu ufuatao:

(a) kumpa chanjo mbwa wake na kulipa ada ya chanjo kama atakavyoelekezwa na Halmashauri;

(b) kuonesha cheti cha chanjo ya mbwa kwa Afisa Mwidhiniwa kabla ya kupata au kuhuisha kibali kilichoisha muda wake;

(c) kumfungia mbwa wake wakati wote wa mchana, kumfungulia kuanzia saa nne kamili usiku na kumfungia saa kumi na moja alfajiri;

(d) kuogesha mbwa kila baada ya siku saba ili kudhibiti magonjwa na wadudu wasumbufu kadri atakavyoelekezwa na Halmashauri; na

(e) kumfunga mbwa kwa mnyororo maalumu wakati wa kutembea nae kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine.

(4) Endapo mfugaji atalazimika kusafirisha mbwa atalazimika kuwa na kasha maalumu la kusafirishia mbwa ambalo ataelekezwa na Afisa Mwidhiniwa kabla ya kupewa kibali.

Mbwa anayezurura

17. Halmashauri inaweza kukamata mbwa atakayepatikana anazurura na kumhifadhi katika kizuizi kwa muda usiozidi siku mbili na baada ya hapo inaweza kumtaifisha au kufanya uamuzi mwingine kadiri itakavyoona inafaa.

Kibali cha kutoa huduma za mifugo

18.-(1) Mtu ambaye anakusudia kutoa huduma za mifugo kwa kuanzisha duka la kuuza vyakula vya mifugo, ghala la kuhifadhia vyakula vya mifugo, kiwanda cha kutengeneza vyakula vya mifugo, kituo cha huduma za

mifugo au zahanati au kituo cha kutotolesha vifaranga katika eneo la Halmashauri atalazimika kupata idhini ya Halmashauri.

(2) Mtu atakayepata idhini chini ya kanuni ndogo ya (1) atapaswa kuwasilisha kwa Afisa Mwidhiniwa taarifa ya robo mwaka ya uuzaji wa vyakula vya mifugo, utengenezaji wa vyakula vya mifugo au ghala, vituo vya huduma za mifugo au zahanati na vituo vya kutotolesha vifaranga.

Makosa

19. Mtu ambaye-
(a) anashindwa au kukataa kuogesha au kuchanja mfugo au mifugo yake ili kuzuia magonjwa;
(b) analisha mfugo au mifugo kwenye maeneo yasiyoruhusiwa;
(c) anaruhusu mfugo au mifugo yake kuzurura hovyo;
(d) anafuga mifugo bila kibali cha ufugaji;
(e) anashindwa au anazembea kutoa taarifa juu ya uwepo wa au dalili za ugonjwa au kifo cha ghafla cha mfugo au mifugo katika banda lake;
(f) anashindwa kutoa ushirikiano wa uwekaji wa alama kwa mfugo au mifugo yake;
(g) anauza na kufuga mfugo au mifugo pembezoni mwa barabara au sehemu ambayo hairuhusiwi;
(h) anasababisha kero ya harufu mbaya na kelele ya mfugo au mifugo yake kwa jamii;
(i) anaanzisha duka la kuuza vyakula vya mifugo, ghala la kuhifadhia vyakula vya mifugo, kiwanda cha kutengeneza vyakula vya mifugo, kituo cha huduma za mifugo au zahanati au kituo cha kutotolesha vifaranga bila idhini ya Halmashauri;
(j) anashindwa kuwasilisha taarifa ya mwezi ya uuzaji wa vyakula vya mifugo, utengenezaji wa vyakula vya mifugo au ghala, vituo vya huduma za mifugo au zahanati na vituo vya kutotolesha vifaranga kwa Afisa Mwidhiniwa;

(k) anaweka vyakula vya mifugo wazi;

(l) anajihusisha na utengenezaji wa vyakula vya mifugo bila kuwa na utaalamu wa vyakula vya mifugo; au

(m) anamzuia Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yak echini ya Sheria Ndogo hii,

anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote.

Adhabu ya jumla

20. Mtu anayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hii ambapo hakuna adhabu mahsusi iliyowekwa, anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu au vyote.

Ufifilishaji wa makosa

21. Mkurugenzi anaweza kumtoza faini mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii, kiasi cha shilingi elfu hamsini iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Nne.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5(d))*

IDADI YA MIFUGO INAYORUHUSIWA KUFUGWA KATIKA ENEO LA HALMASHAURI

| Namba | Aina ya Mfugo | Idadi | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | - | Mfugaji atapewa kibali cha kufuga kulingana na ukubwa wa eneo alilonalo bila kusababisha kero ya harufu na kelele kwa jamii |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2. | Mbuzi au Kondoo | - | Mfugaji atapewa kibali cha kufuga kulingana na ukubwa wa eneo alilonalo bila kusababisha kero ya harufu na kelele kwa jamii |
| 3. | Nguruwe | 4 | Nguruwe Watoto wakiachishwa kunyonya wauzwe au kuondolewa |
| 4. | Mbwa | - | Mfugaji atapewa kibali cha kufuga kulingana na ukubwa wa eneo alilonalo bila kusababisha kero ya harufu na kelele kwa jamii |
| 5. | Wanyama wa jamii ya ndege | - | Mfugaji atapewa kibali cha kufuga kulingana na ukubwa wa eneo alilonalo bila kusababisha kero ya harufu na kelele kwa jamii |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 6(1))*

KIBALI CHA KUFUGA MFUGO

Jina la Mfugaji:………………………………………………………..

Anuani:…………………………………………………………

Kata:…………………………………… Mtaa …………………

Namba Nyumba:…………………………………… Namba Kitalu:……………

Ameruhusiwa kufuga Mifugo ifuatayo katika eneo la ……………………………..

| Na | Aina ya Mfugo | Koo | Idadi ya Mifugo | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Jike | Dume | |
| 1 | Ng'ombe | | | | |
| 2 | Mbuzi | | | | |
| 3 | Kondoo | | | | |
| 4 | Nguruwe | | | | |
| 5 | Ngamia | | | | |
| 6 | Punda | | | | |
| 7 | Paka | | | | |
| 8 | Farasi | | | | |
| 9 | Sungura | | | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 10 | Mbwa | | | | |
| 11 | Kuku au Bata | | | | |
| 12 | Wanyama wengine | | | | |

Kibali hiki kimetolewa kwa Ndugu:………………………………………kwa muda wa miezi/miaka …………….. kwa Mfugo au mifugo kuanzia tarehe……………..hadi tarehe…………..

Kimetolewa na:

Jina la Afisa Mwidhiniwa…………………………………..Saini………

Wadhifa:………………………………………………………………..

Tarehe:…………………

Muhuri:……………………………………………

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 8 (1))*

KIBALI CHA KUSAFIRISHA MIFUGO

Jina:…………………………………………….

Anuani:…………………………………………

Ameruhusiwa kusafirisha Mifugo ifuatayo kutoka ………………kupitia njia za……………………..hadi…………..…..

| Namba | Aina ya Mfugo | Idadi ya Mifugo |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | |
| 2. | Mbuzi | |
| 3. | Kondoo | |
| 4. | Nguruwe | |
| 5. | Ngamia | |
| 6. | Punda | |
| 7. | Paka | |
| 8. | Farasi | |
| 9. | Sungura | |
| 10. | Mbwa | |
| 11. | Kuku au Bata | |

| | | |
|---|---|---|
| 12. | Mifugo mingine | |

Kibali hiki kitakuwa cha muda wa siku….. kuanzia tarehe…....hadi tarehe……….
Kimetolewa na :
Jina la Afisa Mwidhiniwa:……………………………………….
Saini:………………………………………………………..
Wadhifa:…………………………………………………………..
Tarehe:……………………………………………………….....
Muhuri:……………………………………

JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 21)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi …………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, kwamba mnamo tarehe …… ya Mwezi ………. mwaka ……….…… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya …… ya Sheria Ndogo ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ya Mwaka 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, niko tayari kulipa kiasi cha faini badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. ya Mwezi…………..… Mwaka …………….

Jina……………………………….. Saini……………………..

MBELE YANGU:

Jina:…………………………………..……………………

Saini………………………..…………………………..………

Wadhifa:………………………………………………………

Tarehe………………………………………………

*Tangazo La Serikali Na. 506 (Linaendelea)*

Lakiri ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imegongwa kwenye sheria hii kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni uliofanyika tarehe 24 mwezi 08 Mwaka 2023 na kushuhudiwa Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya ;

HANIFA SULEIMAN HAMZA
*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni*

SONGORO KHAMISI MNYONGE
*Mstahiki wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni*

NAKUBALI

L.S

Dodoma
10 Disemba 2023

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wan chi- ofisi ya Rais (Tawala za mikoa na serikali za mitaa)*